OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI WASA

SIMU: +255 0620439952/0719510520 MKUU 0621639887 MAKAMU S. L. P 2149 RUAHA – IRINGA
BARUA PEPE: wasasecondaryschool@gmail.com

KUMB. NA. WSS/1242/J1/16. TAREHE……

MWANAFUNZI……
S/M……..
S.L.P……..
IRINGA.

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WASA KIDATO CHA ……..MWAKA 2021

Ninafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya WASA kwa masomo ya kidato cha **KWANZA** kwa mwaka wa masomo unaoanza tarehe **Januari. 2**020 hongera sana, Ni matumaini yangu unatambua umuhimu wa nafasi adhimu uliyopewa na Taifa ili uisaidie jamii kwa maendeleo.
Shule ipo umbali wa **Kilometa 40** toka njia panda ya Ifunda **[MASUMBO - WASA]** ni shule ya kutwa ingawa kuna nafasi ya Hostel kwa wanao toka mbali na shule. Shule itafunguliwa tarehe **06.01.2020** hivyo unatakiwa kuwepo siku hiyo tayari kwa masomo.
Pia unatakiwa ukamilishe mahitaji na uambatanishe pamoja na fomu zilizojazwa kikamilifu. Ukichelewa zaidi ya **siku 14** nafasi hii atapewa mtu mwingine.

Pamoja na barua hii naambatanisha sheria, kanunina taratibu za shule. Wewe pamoja na mzazi/mlezi wako mnatakiwa kusoma kwa makini sheria, kanuni na taratibu zote zilizoainishwa na ikizingatiwa kuwa kigezo cha maendeleo ya kila mwanafunzi atakayejiunga na shule hii kitalenga katika maendeleo ya **TAALUMA** na **NIDHAMU BORA,** pamoja na kazi za **ELIMU YA KUJITEGEMEA.**

Unapomleta mwanao kusajiliwa shuleni, hakikisha unarudisha nyaraka zifuatazo ;

(a) Fomu ya kukubali masharti ya kujiunga na shule (F.1).
(b) Arudishe fomu ya mwanafunzi kupokelewa shuleni (F.2).
(c) Arudishe fomu ya kukubaliana na mabadiliko ya sharia (F.3)
(d) Arudishe fomu za kupimwa afya (F.4).
(e) Alete nakala ya cheti cha kuzaliwa.
(f) Alete picha 3 za mwanafunzi za rangi (Pass port size), akiwa amevaa sare ya shule.
(g) Alete jalada (File) ambalo litakuwa ni mali ya mwanafunzi kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu/taarifa zake mbalimbali. Na aina ya jalada (File) ni:- Office file A4 320 au PP Folder A4 320 au Tanzania Government. Hatupokei aina hii ya jalada (file); Box file au Spring file au Flat file.

NB: Usajili wa mwanafunzi utakamilika iwapo tu taarifa zote hapo juu zitawasilishwa Shuleni Na Mzazi/Mlezi, siku ya kuripoti.

Ninakutakia maandalizi mema vilevile ninakukaribisha wewe Mzazi/Mlezi hapa shuleni kwa mashauriano kuhusu ufanisi wa kazi yetu. **HONGERA , KARIBU SANA WASA SEKONDARI**

……
MWAKISISYA. A. A
MKUU WA SHULE.

A: MAAGIZO YA JUMLA KWA WANAFUNZI WOTE (KUTWA NA HOSTELI)

1. Aje na Picha tatu (03) “passport size” za langi ya “light” bluu.
2. Counter books quire 3. Zisizopungua tisa (09) kwa ajili ya notisi za masomo darasani
3. Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set), “pen” na “pencil” n.k
4. Vitabu vya ziada kwa ajili ya kujisomea binafsi
5. Kwanja, fagio (02) za chelewa na jembe. Kwa mwanafunzi wa kutwa, **Vifaa hivyo atavitunza mwenyewe anakoishi, ila kwa wanafunzi wa hosteli watakabidhi shuleni ambapo watavitumia kwenye miradi na maeneo yao ya usafi waliyopangiwa kuyahudumia.**
6. Kamsi “dictionary” ya kiingeleza kwa Kiswahili kwa ajili ya kujifunzia misamiati migumu. **(Ni lazima mzazi/mlezi umununulie kitabu hicho ili kumrahihishia mtoto kujifunza misamiati ya lugha ya kiingeleza)**

B: MAHITAJI YA SARE ZA SHULE:

(a) WAVULANA:

1. Awe na suruali 2 (nyeusi na nyekundu damu ya mzee) za kushona zenye malinda 2 na zenye mpindo chini, na mashati 2 meupe mikono mifupi (mitumba marufuku)
2. Viatu vyeusi vya ngozi jozi moja, viwe na visigino vifupi.
3. Soksi aina yeyote jozi mbili.
4. Sweta mbili (moja **BLUU** na nyingine **DAMU YA MZEE**) Anunue mwenyewe.
5. Kofia aina ya mzula ya rangi ya bluu (isiyo na maadishi) **itavaliwa nyakati za usiku.** Kwa ajili ya kujikinga na baridi.
6. Fulana (Tshirt) Nyeupe mbili. Bukta ya bluu na Raba za michezo anunue aje navyo.
7. Shati nyeupe mbili (2) mikono mifupi .
8. **Tracksuit nyeusi** yenye michirizi myeupe mikononi na miguuni na suruari ya rangi ya kaki yenye mpindo chini na lisani mbili kila upande aje nazo, ni sare wakati wa jioni baada ya masomo.

(b) WASICHANA:

1) Sketi mbili za Kijani kibichi na damu ya mzee zenye malinda 12 – 16 za kitambaa kizito. (kitambaa chepesi hakiruhusiwi). Aje nazo zikiwa zimeshonwa.
2) Blauzi nyeupe mbili (2) mikono mifupi.
3) Viatu nyeusi vya ngozi jozi moja viwe na visigino vifupi.
4) Soksi nyeupe jozi mbili.
5) Sweta mbili (moja **BLUU** na nyingine **DAMU YA MZEE**) Anunue mwenyewe.
6) Kofia aina ya mzula ya rangi ya bluu (isiyo na maadishi) **itavaliwa nyakati za usiku.**
7) Fulana (Tshirt) Nyeupe mbili. Bukta ya bluu na Raba za michezo anunue aje navyo.
8) **Tracksuit nyeusi** yenye michirizi myeupe mikononi na miguuni na gauni ya rangi ya pinki yenye urefu wa hadi kongo mbili aje nazo, ni sare wakati wa jioni baada ya masomo.

NB: kwa Wasichana wa Kiislamu, wanaruhusiwa kuvaa mavazi kama ifuatavyo:-

1. Sketi ndefu kabisa usawa wa kongo mbili, rangi zilizotajwa hapo juu. Nusu kanzu nyeupe mikono mirefu
2. Kijuba/hijabu nyeupe isio na urembo ashone mwenyewe. Kijuba/hijabu ya rangi nyingine tofauti na nyeupe hairuhusiwi kabisa, hata wakati wa mapunziko inavaliwa myeupe tu.

   (mavazi hayo, ndio atakayovaa akiwa shuleni ama wakati wa kwenda Msikitini. Mwanafunzi yeyote hataruhusiwi kuvaa vazi lolote tofauti na sare za hapo juu anapotoka nje ya shule).

C: MAGONJWA

Wagonjwa wote shuleni watapata kibali cha kwenda hospitali kupitia Ofisi ya Malezi.

D: USAFI

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku. Zingatia yafuatayo:
a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi yake.
b) usafi wa maeneo yafuatayo kama utakavyopangiwa; ukumbi wa chakula, ukumbi wa mikutano, mabweni, vyoo, madarasa, maabara, viwanja na barabara. Pia vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.

E^ WAGENI

(a) Wageni hawaruhusiwi kufika shuleni kuonana na mwanafunzi wakati awapo masomoni.
(b) Wanafunzi watatembelewa siku ya Jumapili ya kila mwisho wa mwezi kuanzia 8:00 mchana hadi 11:00.
(c) Taarifa za tatizo lolote lile kutoka nyumbani zitolewe kwa uongozi wa shule na siyo mwanafunzi husika moja kwa moja. Namba za simu zipo katika ukurasa wa kwanza.

NB: Wazazi/Walezi watakao watembelea wanafunzi ni wale tu ambao taarifa zao ziko kwenye jalada (File) la mwanafunzi (wengine hawaruhusiwi).

F: DINI/DHEHEBU

(a) Shule inaruhusu kila mwanafunzi kuabudu kulingana na imani ya dini au dhehebu lake linalotambuliwa na Wazazi/Walezi wake, kwa kufuata ratiba na taratibu za shule.
(b) Mwanafunzi hataruhusiwa kubadili dini au dhehebu lake bila ya taarifa rasmi ya maandishi kutoka kwa Mzazi/Mlezi wake yaliyopitishwa na Afisa Mtendaji wake wa mtaa/kata.

G: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE

Binadamu asilani kukaa pamoja si bure wana malengo **MAHUSUSI.** Aidha Taasisi kama hii yetu **INA MALENGO**. Ili kufanikisha malengo hayo, ni lazima kuwe na kanuni, taratibu na sheria maalumu za kufuata, hususani mwanafunzi wa WASA SEKONDARI anapaswa kufuata na kutekeleza kanuni, sheria na taratibu zifuatazo:

a. HESHIMA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:
1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia Darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutotumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayekuita.
8. Kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa “coat of Arms”, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

9. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
12. Kunyosha mkono juu na asimame anapouliza na kujibu maswali.
13. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
14. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.

b. MAHUDHURIO

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba na madarasa.

c. MAANDALIO YA JIONI

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni kuanzia saa 1.30 hadi saa 4.00 usiku. **Mwanafunzi harushusiwi kukaa au kulala bwenini muda huu, ukipatikana adhabu kali itatolewa zidi yako.**
2. Timu maalumu ya Walimu watakuwa wanasimamia mahudhulio ya jioni.
3. kila mwanafunzi atatakiwa kudumisha hali ya Utulivu, nidhamu ya hali ya juu, n.k katika masomo ya jioni. Hii itamsaidia kusoma kina na kwa upana kwa kile alichopanga kusoma.

d. MAENDELEO YA MWANAFUZI KITAALUMA NA TABIA

Shule hatuna taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia na kitaaluma kila mwezi, bali kila mwisho wa nusu mhura na mwisho wa mwaka, tafadhali mzazi/mlezi hakikisha unaipata kila mwisho wa nusu mhura na kumshauri mwanao kuhusu maendeleo yake.

e. KUWAHI

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuthamini muda.
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa kufuatana na muhula husika.

f. SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:

1. Masomo darasani
2. Kutoka nje ya shule Kwa shughuli za kishule ama binafsi endapo amepewa ruhusa ya kutoka nje.
3. Baraza la shule.
4. Kwenda hospitalini.
5. Kwenda maandamano.
6. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo.
7. Kazi za mikono (vazi la kazi).
8. Michezo.

NB: Mwanafunzi haruhusiwi **kujaa na nguo za nyumbani** nje ya zile ulizoagizwa na shule au **Kuvaa kofia, nguo fupi, zenye mipasuo, kufuga kucha ndefu, kupaka rangi kucha na midomo, kuvaa heleni, mikufu, bangili, nguo za kubana, viatu visivyo vya shule, mapambo mengine yoyote pamoja na sare akiwa shuleni.**

g. MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:

i. Chumba cha walimu (staffroom).
ii. Ofisi za shule.
iii. Maabara.
iv. Jikoni.
v. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

H: MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro/kulala nje ya shule bila ruhusa
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

---

5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
7. Kufuga ndevu
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya lulevya
9. Uvutaji wa sigara
10. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
11. Kupata ujauzito au kutoa mimba
12. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
16. Kudharau bendera ya taifa.
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
18. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
19. kumiliki simu mazingira ya shule.
20. Kugoma adhabu

FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE (F.1)

SEHEMU YA MWANAFUNZI

I. Mimi _____ kidato cha _____ninakubali kujiunga na shule ya sekondari Wasa nikiwa mwanafunzi wa Hosteli/kutwa

II. Ninakubali masharti yote na ninaahidi kufuata sheria zote za shule.

III. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi _____ Tarehe _____

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi _____ ninakubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari Wasa kuanzia tarehe _____, akiwa mwanafunzi wa **hosteli/kutwa** (kata isiyo husika) . Ninakubali masharti yote yaliyomo katika maelezo ya kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na **kulipa gharama za uharibifu wa mali za umma ikwa mwanafunzi amefanya uharibifu huo kwa makusudi** na kumtimizia mahitaji mengine ya shule. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa ana afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi/mlezi mwenyewe.

(a) Anuani yangu ya kudumu ni:-

_____

_____

_____

(b) Jina na anuani ya mlezi wa karibu mkoa wa Iringa/ kijiji cha Wasa ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbalimbali ya mtoto ni:-

FOMU YA MWANAFUNZI YA KUPOKELEWA SHULENI

1. Jina kamili la mwanafunzi **……..……**
2. Mahali ulipozaliwa **……**
3. Tarehe ya kuzaliwa **……**
4. Uraia **…….…….**
5. Anwani ya nyumbani **……..…..…. …**
6. Anwani ya mzazi (kama tofauti na hiyo hapo juu) **……..….. ..**
7. Jina la mzazi/mlezi **……**
8. Kazi ya mzazi/mlezi **……..…**
9. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi **……..… ..**

Huu ni mfano wa namna ya kujaza hapo chini

Jina	**Uhusiano**	**Anuwani**	**Simu**
Akili Mkwa	Baba	S.L.P. 145, Iringa	0262702096

PICHA YA BABA

Jina	**Uhusiano**	**Anwani**	**Simu**
(a) ……..	…….	……	…… …
(b) ……..	…….	……	……
(c) ……..	…….	……	……
(d) ……..	…….	……	…… ..

PICHA YA BABA

PICHA YA MAMA

N.B: Ndugu walioandikwa ndio wanapaswa kushughulikia masuala ya nidhamu, maendeleo na uhamisho wa mwanafunzi husika tu. Iwapo kutatokea mabadiliko kwa sababu yoyote ile, taarifa iletwe shuleni ili kufanyike mabadiliko hayo.

10. Dini **……. ……**
11. Kidato ulichopokelewa ……. ……
12. Shule uliyotoka ……. ……
13. Shughuli unazozipendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k.

14.Wilaya unayotoka …….. Mtaa ……. Kata…… ……
15.Jina la M/kiti wa kitongoji/mtaa…… ...……..simu……mhuri wa kijiji……
16. Jina la mtendaji wa Kijiji/Mtaa……simu…….....mhuri……...
17. Sahihi ya Mwanafunzi ……..…. Tarehe ……. …….

TAARIFA YA MABADILIKO YA ADHABU KWA WANAFUNZI KUANZIA F.3 JANUARY 2019 KWA MWANAFUNZI ATAKAYEKAMATWA NA SIMU SHULENI

1. UTANGULIZI

Shule kama taasisi ni lazima iwe na sheria, kanuni na taratibu za kufuata ili malengo ya kitaaluma yaweze kufikiwa.

2. MAELEKEZO

Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978, sheria ya Elimu namba 5 ya mwaka 2007 na kanuni ya nne ya Elimu ya mwaka 2014, zimeainisha bayana makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kusimamishwa au kufukuzwa shule.

Bodi ya shule kama chombo kilichoundwa kisheria bado kinaendelea kutekeleza matakwa ya sheria hizi, kwa kuzingatia sheria ya Elimu namba 10 ya mwaka 1995, iliyotoa mamlaka kwa Bodi ya shule kushughulikia nidhamu za wanafunzi.

Aidha kutokana na sheria ya Elimu namba 5 ya mwaka 2007, inayotoa mamlaka kwa Bodi ya shule kufanya mabadiliko ya sheria, kanuni na taratibu za shule. Bodi ilifanya kikao tarehe 23 .11.2018 na kufanya mabadiliko kwa baadhi ya adhabu zilizokuwa zikitolewa kwa wanafunzi ikiwemo matumizi ya simu shuleni, baada ya kubaini kuwa tatizo hili limekuwa sugu kwa wanafunzi. Mabadiliko hayo ni kama yafuatayo:-

(i) Mwanafunzi atakayekutwa na simu shuleni au kifaa chochote cha simu, ataadhibiwa kwa kurudishwa nyumbani kwa siku 14 na kuleta bati tatu (03) za geji 28 siku Mzazi/Mlezi wake anapomrejesha shuleni.

3. AHADI YA KUKUBALI MABADILIKO YA ADHABU

Nimesoma, nimeelewa, nimekubaliana na mabadiliko ya adhabu yaliyowekwa na Bodi ya shule. Ninaahidi kwamba, **nipo tayari kutumikia adhabu hizo/nipo tayari kwa mwanangu kutumikia adhabu hizo** (kata lisilokuhusu), mara itakapobainika kufanya makosa yaliyotajwa hapo juu.

(i) Jina la mwanafunzi _____ Kidato _____ Mkondo…….
Sahihi _____ Tarehe _____

(ii) Jina la Mzazi/Mlezi _____ Namba ya simu _____
Sahihi _____ Tarehe _____

(iii) Mtaa/Kitongoji /Kijiji _____ Kata _____
Wilaya _____Mkoa_____

4. SHAHIDI WA AHADI

(i) Jina la Afisa Mtendaji wa Mtaa /kijiji _____
Namba ya simu _____Sahihi _____ Tarehe_____ Muhuri _____

(ii) Jina la Afisa Mtendaji wa Kata _____
Namba ya simu_____ Sahihi _____ Tarehe _____ Muhuri _____

TANBIHI: Fomu hii irudishwe shuleni ikiwa imesainiwa na wahusika wote.

MKUU WA SHULE

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

MEDICAL EXAMINATION FORM

WASA SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 2149,
RUAHA-IRINGA
……

To
THE MEDICAL OFFICER,
……..
……..
……..
Please examine…….
As to her fitness for pursuing further education at this school.

1. Haemoglobin ……
2. P.V. Bleeding …….....
3. (a) Sight defect ……
(b) Hearing……
4. Blood Pressure……
5. Urine for Sugar and Pregnancy test……
6. Stool for routine examination……
7. Asthima……
8. Skin diseases……
9. Leprosy ……..
10. Epilepsy……
11. Pulmonary tuberculosis…….
12. Deformity……..
13. Mental Problem……
14. Comments……

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by the Medical Officer)
I have examined the above named and consider that she/he is mentally and physically fit for studies.
Signature …… Date ……
Designation ……. Station ……...

NB :Fomu hii irudishwe kwa Mkuu wa Shule ikiwa imejazwa kikamirifu

MWAKISISYA. A. A.
MKUU WA SHULE.